# Umilisi Kimsingi wa Mashairi na Namna Unavyoathiri Ufasiri na Uelewekaji wa Ushairi katika Shule za Upili

*Gakuo Joseph Kariuki*
*Chuo Kikuu cha Kenyatta*

**Ikisiri**

**Makala haya yanachunguza changamoto za ufasiri na uelewekaji wa mashairi miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa sekondari nchini Kenya. Tunahoji kwamba ukosefu wa umilisi kimsingi kuhusu taaluma ya ushairi ni sababu kuu inayopelekea wanafunzi wengi kutomakinika katika somo la mashairi. Tunaegemeza tathmini yetu katika mihimili ya nadharia mseto hususan; ya Uhementiki na ya Uhistoria Mpya. Nadharia ya Uhementiki inadai kwamba ili kuelewa matini nzima, sharti sehemu zote za matini husika zieleweke. Kadhalika, ili kufasiri kila sehemu ya matini kwa ufasaha,sharti mfasiri azingatie matini nzima. Nadharia ya Uhistoria Mpya hutoa msingi maridhawa wa uchambuzi wa matini katika miktadha ya kihistoria. Inaelekeza kuwa; mwingiliano matini uliopo unapatikana kwa kuitazama jamii, mazingira, historia na utamaduni wa jamii husika na wala, si lazima mhakiki au mfasiri ajifunge kwenye kipengee fulani maalum pekee cha kazi hiyo kama vile lugha. Ni matumaini yetu kuwa makala haya yatatoa kurunzi kwa washika dau kukabiliana na uto-umilisi katika taaluma ya ushairi jambo ambalo tunaamini fika kuwa litasaidia kuondoa kiwi la kutoeleweka kwa ushairi miongoni mwa wanafunzi hao katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.**

**Maneno Muhimu**: Mashairi, Umilisi, Athari, Shule Za Upili, Ufasiri

## Utangulizi

Makala haya yanachunguza na kuaangazia changamoto ya ukosefu wa umilisi kimsingi kuhusu ushairi wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari nchini Kenya. Umilisi kimsingi ni ujuzi ambao wanafunzi au wasomi wanao au wanatarajiwa kuwa nao kuhusu taaluma wanayojifunza. Umilisi kimsingi wa ushairi wa wanafunzi wa sekondari ambao wamejiunga na kitengo hicho cha usomi ni maarifa ambayo tayari wanayo au wanafikiriwa kuwa nayo kuhusu ushairi. Maarifa hayo hutokana na mafunzo na tajriba zao walizopata kuhusu ushairi katika shughuli zao za usomi.Tunatumia kielelezo cha kaunti mbili ya Trans Nzoia, na Mombasa kuonyesha changamoto zinazotokana na ukosefu wa umilisi kimsingi hususan katika kuendelea kujifunza taaluma ya ushairi. Changamoto hizo ndizo baadhi ya sababu zinazofanya ushairi kuonekana


kama uwanja mgumu wa kiakademia (Gibbe: 1978, 1990). Pamoja na kwamba zipo changamoto nyingi zinazokumba ufasiri na uelewekaji wa ushairi wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi hao wa sekondari kama vile: ukosefu wa muelekeo wa ufundishaji na ujifundishaji ushairi, mielekeo hasi kuhusu ushairi, uhaba wa walimu, ukosefu wa vitabu vya kiada na utahini wa kuyumbayumba miongoni mwa zingine nyingi, tatizo la ukosefu wa umilisi kimsingi hutinga usomi wa ushairi kwa kiasi kikubwa.

Tunahoji hapa kwamba uhaba huu wa umilisi kimsingi, ni sababu kuu ya wanafunzi wengi kutomakinika katika somo la ushairi. Kadhalika, upungufu huu unachangia pakubwa kutokuelewa kwa wanafunzi hao ambao huogopa mashairi na kuwafanya kuwa na mielekeo hasi kuhusu taaluma ya ushairi. Tatizo hili sawa na matatizo mengine kama asemavyo Kimaru (2010), na Gakuo (2014), halina budi kutafutiwa suluhisho la kudumu ili wasomi na walimu wa ushairi wazidi kuendeleza utanzu wa ushairi wenye adhama na historia kongwe zaidi miongoni mwa tanzu zingine za fasihi ya Kiswahili. Ili kutathmini suala hili la umilisi kimsingi, tunayatumikiza mashairi ya kimsingi kabisa kutoka kwa vitabu teule vya kidato cha kwanza na cha pili kuona ni jinsi gani wanafunzi wa Kiswahili wanaosomea katika shule za kategoria mbalimbali nchini Kenya wanavyoyafasiri mashairi na ushairi kwa jumla. Uhusishaji huu unafanyika kutokanana zoezi la kazi mradi kwa wasomi hao pamoja na hojaji.

### Uhusishi Viwango


Uchunguzi unadhihirisha kwamba hamna tofauti kubwa miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili katika shule za sekondari kuhusu usuli na ufasiri wao wa mashairi kimsingi. Tofauti hudhihirika mwishoni mwa masomo kutegemea ubora wa ufundishaji na ujifundishaji wa mshairi.

### Kategoria ya shule





Asilimia hamsini ya wanafunzi wasailiwa wa shule katika kaunti za Trans Nzoia na Mombasa walikuwa ni wa kategoria ya shule za kitaifa. Wale wa shule za kategoria ya Mkoa na Wilaya (yaani kaunti kama ilivyojulikana awali), walikuwa asilimia ishirini na tano kila moja.

**Jinsia**




Kama mchoro unavyobainisha, uchunguzi wetu ulihusisha viwango vilivyo sawa vya kijinsia wasichana kwa wavulana katika kidato cha tatu na cha nne yaani asilimia 50 kila jinsia.

**Kidato**




Uchunguzi ulilenga kidato cha tatu na cha nne kwa kiwango sawa yaani, asilimia hamsini ya wasailiwa walitoka katika kila kidato (cha tatu na cha nne).Katika kuangazia ujuzi waliokuwa nao wanafunzi hao (umilisi kimsingi) kuhusu mashairi, walihusishwa katika kukamilisha hojaji kuhusu hali na uelewa wao wa ushairi Hojaji hizi ziliazimia kukadiria ugumu wao wa kuelewa na kuhakiki mashairi. Hasa, walihojiwa kuhusu kiini cha ugumu wa kuelewa na kufasiri mashairi na maoni yao kuhusu walichokiona kama kiini cha ugumu huo. Isitoshe, matokeo yao katika mitihani ya ushairi yalichunguzwa.

**Walipoanza kusoma mashairi**

| **Asili ya masomo kuhusu ushairi** | **Idadi marudio** | **Asilimia** | **Asilimia Limbikizi** |
|---|---|---|---|
| Katika shule ya Msingi | 34 | 85.0 | 85.0 |
| Katika shule ya Sekondari | 6 | 15.0 | 100.0 |
| Jumla | 40 | 100.0 | |

Kigezo hiki cha walipoanza kusoma ushairi, kinatoa maelezo muhimu kuhusu wakati wanafunzi wasailiwa walianza kujifunza somo la mashairi. Inadhihirika kuwa asilimia 85 ya wanafunzi wasailiwa walianza kujifunza mashairi na ushairi wakiwa katika shule ya msingi. Asilimia 15 ya wanafunzi hao wasailiwa walianza kukabiliana na somo la mashairi katika shule ya sekondari. Hiki ni kiwango kikubwa sana cha wanafunzi ikichukuliwa kuwa kielelezo hiki ni cha taifa zima la Kenya. Ni kiwango hiki cha walipoanza kusoma ushairi ambacho tunalenga katika makala haya, kuona ni vipi tunaweza

kukabiliana na changamoto yake ya ufasiri na uelewa wao kuhusu ushairi wa Kiswahili.

**Wanavyolichukulia somo la mashairi**

| | **Idadi marudio** | **Asilimia** | **Asilimia Limbikizi** |
|---|---|---|---|
| Nalipenda | 31 | 77.5 | 77.5 |
| Sina Uhakika | 4 | 10.0 | 87.5 |
| Silipendi | 5 | 12.5 | 100.0 |
| Jumla | 40 | 100.0 | |

Wanafunzi wengi (Asilimia 77.5) walielekea kulipenda somo la ushairi ilihali asilimia 12.5 kati yao hawakulipenda. Asilimia 10 kati ya wasailiwa wote walidhibitisha kutokuwa na hakika kuhusu walivyolichukulia somo la mashairi. Uchunguzi ulibainisha asilimia zaidi ya 22.5 ya wanafunzi hao kuwa na umilisi kimsingi wa ushairi wa kutamausha. Upungufu huo wa kiumilisi kama tulivyodokeza katika utangulizi, ndio kiini cha muelekeo hasi kuhusu ushairi miongoni mwa wanafunzi hao.

**Makadirio ya uelewa wa mashairi**

| | Idadi marudio | Asilimia | Asilimia Limbikizi |
|---|---|---|---|
| Naelewa sana | 2 | 5.0 | 5.0 |
| Naelewa kiasi | 37 | 92.5 | 97.5 |
| Sielewi | 1 | 2.5 | 100.0 |
| Jumla | 40 | 100.0 | |

Kigezo hiki cha makadirio ya uelewa wa mashairi, kinashamiria uelewa wa wanafunzi kuhusu ushairi na mashairi. Kinabaini kuwa ni asilimia 5 tu ya wanafunzi wote walioelewa sana somo la mashairi. Asilimia 92.5 wanayaelewa kwa kiasi huku asilimia 2.5 wakiwa hawalielewi kabisa somo la ushairi. Kwa jumla, ushairi ni taaluma ngumu kwa karibu wasomi wengi. Ni takribani wanafunzi asilimia 10.3 pekee wanaoliona somo la ushairi kuwa rahisi kama jedwali linalofuatia linavyoonyesha:

**Kuhusu ugumu wa mashairi**

| | **Idadi marudio** | **Asilimia** | **Asilimia Limbikizi** |
|---|---|---|---|
| Magumu sana | 3 | 7.7 | 7.7 |
| Magumu kiasi | 32 | 82.1 | 89.7 |
| Rahisi | 4 | 10.3 | 100.0 |
| Jumla | 39 | 100.0 | |

Kuhusu wanafunzi kuelewa kiini cha ugumu wa mashairi, asilimia 56.8 wanadai ugumu wa mashairi unatokana na mashairi yenyewe. Asilimia 18.9 ya wanafunzi hao wanahusisha ugumu wa mashairi na wao wenyewe kutoyafahamu na kutoyamakinika mashairi na ushairi kwa jumla.

**Kiini cha Ugumu wa mashairi**

| **Sababu ya ugumu** | **Idadi marudio** | **Asilimia** | **Asilimia Limbikizi** |
|---|---|---|---|
| Mashairi yenyewe | 21 | 56.8 | 56.8 |
| Mimi Mwenyewe | 7 | 18.9 | 75.7 |
| Ufundishaji | 8 | 21.6 | 97.3 |
| Sina uhakika | 1 | 2.7 | 100.0 |
| Jumla | 37 | 100.0 | |

Ugumu huo unaathiri matokeo yao katika mitihani ya ushairi kama inavyoakisiwa na jedwali linalofuata:

**Matokeo ya mtihani**

| | **Idadi marudio** | **Asilimia** | **Asilimia Limbikizi** |
|---|---|---|---|
| Mazuri sana | 1 | 2.6 | 2.6 |
| Mazuri | 18 | 46.2 | 48.7 |
| Wastani | 19 | 48.7 | 97.4 |
| Chini ya wastani | 1 | 2.6 | 100.0 |
| Jumla | 39 | 100.0 | |

Wanafunzi asilimia 2.6 tu ndio walioungama kuwa na matokeo mazuri sana. Asilimia 46.2 walikuwa na matokeo mazuri kiasi, wakati ambapo asilimia 48.7 walikuwa na matokeo ya wastani katika ushairi. Jumla ya wanafunzi asilimia 2.6 walipata matokeo chini ya wastani. Hili la matokeo katika mtihani ndilo tulilotathmini kupitia kazi mradi kwa kuhusisha mashairi ya kawaida kutoka vitabu teule vya kidato cha kwanza na cha pili.

**Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Kwanza**

Baada ya kuvipitia vitabu hivi, tuling'amua kwamba kufikia 2014, wanafunzi walipewa mafunzo machache kuhusu ushairi katika kidato cha kwanza. Tulitambua mashairi matatu yaliyohusishwa na somo la ufahamu. Mashairi hayo ni "Gogo" (Uk. 48), "Malenga Mlotukuka" (Uk. 99) na "Mavazi Rekebisheni" (Uk. 120). Mashairi haya yalitumika kama kigezo cha kutathmini umilisi kimsingi wa ufasiri na uhakiki wa Ki-Hemenitiki na Uhistoria Mpya wa ushairi wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi hao.

Ijapo tulielewa fika kwamba mashairi ya Kiswahili sawa na matini mengine hayana fasiri rasmi, na kwamba wanafunzi tofautitofauti wangeyafasiri mashairi hayo kwa njia tofautitofauti kulingana na uelewa wao wa kibinafsi, tathmini iliegemezwa kwenye vigezo vya ufasiri mwafaka wa Ki-Hemenitiki. Vigezo hivyo vilitumiwa kubainisha mambo yafuatayo: ukubalifu, uwiano, ufaafu na mshikamano kama yanavyoelezewa na Hirsch (1987).

Vigezo hivi tulivyooanisha na mihimili sita ya nadharia ya Ki-Hemenitiki ambayo ni:

a) Kutalii matini kama mjadala ulio wazi baina ya msomaji mpya na historia ya fasili
b) Uwezekano wa matini kuleta maana iliyokusudiwa au kuipotosha maana hiyo
c) Uwezekano wa baadhi ya wasomaji kuelewa ilihali wengine wakatatizikaa kuelewa maudhui
d) Uhusiano wa mtunzi na kazi yake
e) Uchambuzi wa matini/shairi zima
f) Uwezekano wa kutoeleweka kwa matini/shairi lenyewe

Kuhusu nadharia ya Uhistoria Mpya, tulihusisha suala la muktadha wa kijamii unavyoingiliana na kazi ya fasihi. Uchunguzi uliegemea vilevile mihimili sita ya nadharia hii ambayo ni pamoja na:

a) Uchunguzi wa muktadha halisi wa jamii ya mwandishi na unavyoingiliana na kazi yake
b) Jinsi utamaduni unavyoingiliana na maendeleo ya kazi husika za jumuiya husika
c) Namna wakati wa upokeaji wa kazi unavyoakisi fasihi
d) Jinsi mazingira ya mtunzi yanavyoathiri dhamira za kazi yake
e) Namna muktadha wa kihistoria unavyoakisi chimbuko la kazi ya fasihi
g) Jinsi ya kutazama upya muktadha wa kijamii pamoja na utamaduni

Malengo haya yanayooana na mihimili hii sita ya nadhaira ya Uhemenitiki na Uhistoria Mpya ndio yalikuwa kiini cha uchunguzi huu. Isitoshe,tulitalii vilevile hatua za uchambuzi wa Uhistoria Mpya hususan: uzingatiaji wa muktadha wa historia ya chimbuko la kazi yenyewe, uelezaji wa dhamira za mtunzi, uzingatiaji wa historia ya wakati wa upokeaji wa kazi husika na uchunguzi wa hadhira ya baadaye kwa urazini huku tukifafanua madhumuni na eneo la uhakiki huo.

Tuliliteua shairi "Gogo" lifuatalo na maswali yake ambata.

**GOGO**

Umezuka moto kweli, misitu yateketea,
Wachanji wameduwili, hakuna pa kukimbia,
Zimewakwama akili, mashoka yanaungua,
Gogo linawaka moto, wachanji **tahadharini**.

Kwa kweli kila mahali, halaiki yaumia,
Si Kenya si Shelisheli, mamia yaangamia,
Shikeni yangu kauli, msije kujijutia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Ijapokuwa **kalili**, muda wa kuhadithia,
Yapimeni kwa ratili, haya ninayowambia,
Sijegeuka **shubili**, tamu mnayodhania,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Moto huno ni**kikuli**, hauchomi kuchagua,
Hauna jaji wakili, kwamba utajitetea,
Huchoma kiwiliwili, **pingiti** likasalia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

We mchanji kaa tuli, boresha yako tabia,
**Kugwenya** lile na hili, magongo **kujisombea**,
Twaja tujipige wali, siku ya kukufukia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

Ili wepuke muhali, usije kujililia,
Gogo ulo na kibali, chanja ulilozowea,
Usiyachanje mawili, **zani** utajibwagia,
Gogo linawaka moto, wachanji tahadharini.

**Maswali**

1. Shairi hili ni la aina gani?
2. Eleza vina vya shairi hili.
3. (a) Mizani ni nini?
   (b) Shairi hili lina mizani ngapi katika ubeti wa tatu mshororo wa kwanza?
4. Taja kibwagizo cha shairi hili.
5. Eleza gogo linalozungumziwa na mshairi.
6. Taja nchi mbili zilizotajwa katika shairi.
7. Mshairi ametumia uhuru wa kishairi. Eleza huku ukitolea mfano kila maelezo.
8. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi.

| | |
|---|---|
| Tahadharini | Pingiti |
| Kalili | Kugwenya |
| Shubili | Kujisombea |
| Kikuli | Zani |

**Majibu**

*Shairi hili ni la kijazanda. Gogo linalozungumziwa ni ugonjwa hatari wa UKIMWI ambao mtunzi anaunasibisha na moto unaoramba msitu wote bila ya kusazwa gogo hata moja. Wenye kupenda uroda wamelinganishwa na wachanji wanaotumia mashoka. Mtunzi anatoa tahadhari kwamba tauni hii inatishia kuangamiza siyo tu halaiki bali kizazi cha binadamu kote ulimwenguni.*

*Moto huo umepewa sifa za kitaswira ikiwa ni pamoja na hauchomi kuchagua, hauna jaji wala wakili na kwamba, huchoma kiwiliwili kikasalia pingiti yaani gofu au kifyefye. Mtunzi anatoa wosia kwa hadhira ya wasomaji kurekebisha tabia hasa inayohusu ugwenyaji wa "gogo" hili na lile. Katika ubeti wa mwisho mtunzi anashauri waja kujikita katika silisili za ndoa, yaani kutosheka na kuridhika na mpenzi halisi wa ndoa. Hii ndiyo inayompelekea kushadidi ubeti wake wa mwisho.*

*Shairi hili lilikuwa la kupendeza na kazi ya sahili kwa wanafunzi wa kidato cha tatu na nne. Ni dhahiri kwamba walifahamu na kukubaliana na maudhui yake huku wakionyesha uelewa wao wa mashairi kwa jumla. Wengi wao walikumbuka ukweli waliokuwa wamefundishwa katika shairi hili lenye nia ya kuelimisha kuhusu maswala ibuka bila ya kughafilika.Hata hivyo, kwa wale waliolimatia au kukosa umilisi kimsingi, shairi hili liliwawia kama usiku wa kiza.*

### Kiswahili Fasaha Kwa Kidato Cha Pili

Katika kidato cha pili, nakala ya *Kiswahili Fasaha* kwa kidato cha pili imesheheni kazi nyingi za ushairi kwa wanafunzi hao. Tulipodurusu kitabu hiki, tuligundua kuwa mengi ya mashairi yaliyomo humo ni ya mtunzi Sheikh Shabaan Robert likiwemo shairi maarufu "Kiswahili" uk. 106-107 (*Pambo la Lugha*), "Utenzi wa Hati" uk. 88, "Utenzi wa Adili" (uk. 89) na "Dunia" (uk. 92). Pia, kulikuwemo mashairi mengine yakiwa ni pamoja na Ngonjera "Mwenye Nyumba na Mhitaji" (uk. 30), "Utamaduni kitu gani" (uk. 82), na "Chemsha Bongo" (uk. 99).

Shairi la Shaaban Robert "Dunia" lilitumika katika kutathmini umilisi kimsingi wa ushairi kwa wanafunzi hao. Uamuzi huu ulitokana na maudhui, ukuu wa mtunzi pamoja na lugha yake. Tulitumia mhimili wa nadharia ya Ki-Hemenitiki unaochunguza mtunzi na mhimili wa nadharia ya Uhistoria Mpya unaolenga kuchunguza mtunzi, muktadha na mazingira ya kazi husika. Shairi hili lina beti saba zifuatazo:

### Dunia

Ukitazama dunia, umbo lake huarifu,
Kuwa imeandaliwa, wageni watukufu,
Tayari kuwapokea, na mambo sufufu,
Ndani yake yamejaa, viumbe kuwanadhifu.

Umbole huonyesha, namna lilivyotimu,
Yangoja kukaribisha, katika mastakimu,
Yenye kila tamasha, machungu na matamu,
Maisha yanapokwisha, huiacha inadumu.

Ajae ardhi hii, kutoka katika mimba,
Mzizini au yai, au katika kitumba,

Milki hakinai, ya mali wala mashamba,
Mwisho wa uhai, kaburi lake jembamba.

Halii choyo kaburi, mtu uzima ukisha,
La upana shubiri, urefu pima yatosha,
Wala hadai fahari, tena kujifaharisha,
Akiwa hai fikiri, anavyopenda tamasha!

Yalipo maziara, masikani ya maiti,
Huonyesha ishara, na pengine tofauti,
Dhaifu na bora, hawagombi hawateti,
Wazima kila mara, pato linawasaliti.

Mtu hashibi pato, hili huonyesha nini?
Laonyesha kama pito, kuwa yumo safarini,
Enda kuitika wito, bora usio kifani,
Ambao kila mtoto, wa Adam hutamani.

Yumo katika safari, kila mwanadamu,
Haraka au usiri, kwenda imelazimu,
Epusha roho Kahari, yake na Jahanamu,
Iwe katika fahari, mwili ukiwa kuzimu.

**Maswali**

1. Fafanua sifa za dunia kwa mujibu wa mtunzi.
2. Eleza ushauri wa mwandishi kwa waja kuhusu dunia.
3. Fafanua kwa kifupi kuhusu maisha na mazingira ya mtunzi (Shaaban Robert).

**Majibu**

*Shairi hili linabainisha falsafa na msimamo wa Shaaban RobertMtanzania kuhusu maisha na dunia tunamoishi kama tujuavyo. Mtunzi Sheikh Shabaan Robert alikuwa mtu mwadilifu na mcha Mungu. Aliona dunia kwa jicho la mpito tu. Kwake binadamu ni wasafiri tu duniani. Utajiri wa kweli ni ule wa kiroho yaani kumcha Mwenyezi Mungu na kutazamia maisha ya kweli yajayo baada ya kiama. Kwa shairi hili, mtunzi anategua kitendawili cha maisha na dunia hii. Kwa maoni yake, dunia imeumbwa kupokea "wageni" wote wanaozaliwa humo. Dunia imejaa tamasha za machungu na matamu kwa kila kiumbe. Lakini ukwasi wake huisha pale ambapo kiumbe anafikia mwisho wa aushi na uhai wake.*

*Wakati mja akiwa hai, hujibidiisha kuzimbua riziki na kujilimbikizia milki kwa ambavyo kamwe hakinai. Mtunzi anadhihaki jitihada za mja kama huyo pale ambapo anasema kuwa mwisho wake ni kaburi jembamba ikilinganishwa na mawanda ya mapande ya rasilimali aliyojitwalia. Rasilimali hizo ni pamoja na mali tumbitumbi na mashamba madalbazari. Katika mauko, kuna udhaifu na*

*wasiwasi, utoshelevu na unyenyekevu. Hiki ndicho kiini cha mtunzi kukariri ubetiwa nne na tano.*

*Hatima ya wosia huu mtunzi anatumia kunga ya maswali kuitafakarisha hadhira yake ya wasomaji kuhusu mpito wa maisha. Maisha ni safari. Mara kiumbe huitwa na muumba wake. Hii ndiyo hatima ya kila binadamu. Mtunzi anatoa tumaini kwa waja kuwa huko nako waendako waitwao waitwapo na waitikiapo kuna maisha. Yapasa mja kumwamini Mungu na kumwomba amwepushe na balaa ya kuingizwa Jehanamu.*

*Kwa ujumla, wanafunzi wengi walibaini maudhui ya shairi hili isipokuwa hawakuwa na habari zozote kuhusu mtunzi wake (Shaaban Robert), na mazingira pamoja na falsafa yake kama inavyodhihirika katika matokeo ya kazi mradi yanayofuatia;*

**Matokeo Ya Uchunguzi Wa Umilisi Kimsingi Wa Mashairi**

| **SHAIRI 'GOGO'** | | **SHAIRI 'DUNIA'** |
|---|---|---|
| A B<br>(1) 2 2 2 | | A B<br>(1) 10 8 7 |
| (2) 2 2 2 | | (2) 10 6 5 |
| (3) 2 2 2 | | (3) 2 0 0 |
| (4) 2 2 1 | | (14)63% (12) 55% |
| (5) 2 1 2 | | |
| (6) 2 2 2 | | |
| (7) 2 2 2 | | |
| (8) 8 6 5 | | |
| (22) (19)86% (18)81% | | |
| A = Kaunti ya Trans Nzoia | | |
| B = Kaunti ya Mombasa | | |

**Maelezo**

Jedwali hili linadhihirisha matokeo ya tathmini ya Umilisi Kimsingi wa ushairi. Herufi 'A' inawakilisha tathmini ya Umilisi Kimsingi wa ushairi kwa wanafunzi wa kaunti ya Trans Nzoia ilihali, 'B' inawakilisha ya wale wa kaunti ya Mombasa. Matokeo yake yameratibishwa shairi baada ya shairi.

Katika shairi la kwanza ('Gogo'), wanafunzi wa kaunti zote mbili walipasi vyema sana. Wa kaunti ya Trans Nzoia waliongoza kwa asilimia 86 ilihali, wa Mombasa walipata asilimia 81. Hiki ni kiwango cha juu cha umilisi kimsingi kuhusu ushairi kwa wanafunzi wenye umilisi huo.

Maswali katika mashairi haya mawili yalijikita katika maarifa na ujuzi wao wa jumla kuhusu mashairi. Shairi la pili ("Dunia"), lilihusisha ukengeushi wa Ki-Hemenitiki, yaani, matatizo yanayoweza kuibuka kutokana na ufasiri mbaya wa mashairi. Hali hii ilitokana na mhimili uliolenga habari kuhusu mtunzi wake

(Shaaban Robert). Hali hii ilitokea katika swali la tatu ambapo wanafunzi wa kaunti zote mbili walizoa alama sufuri katika swali hilo lililosheheni alama mbili. Hali hii ilipelekea kiwango duni cha alama za jumla kuhusu shairi 'Dunia'. Ni majibu kutokana na suali hili yanayodhihirisha athari kubwa ya umilisi kimsingi katika ufasiri na uelewekaji wa ushairi. Kwamba mwanafunzi atakosa ujuzi au umilisi huu kimsingi katika kiwango chochote kile cha usomi hasa katika shule za msingi na,au, katika kiwango cha kimsingi cha sekondari (kidato cha kwanza na cha pili). Mstakabali wake katika kumudu ushairi utakuwa wa kuyumbayumba.

Matokeo haya yanadhihirisha kuwa baadhi ya wanafunzi wa sekondari hawana umilisi kimsingi wa mashairi. Pia kuna kutokuelewa kiini cha wasilisho la mtunzi katika shairi. Hali hii huibua ugumu usiokadirika kwa wanafunzi kufasiri na kuelewa ushairi. Tunapendekeza ufaulishaji wa ufasiri na uelewekaji wa ushairi miongoni mwa wanasekondari utokane na ufundishaji na ujifunzaji mashairi katika kiwango cha kimsingi cha masomo kuanzia chekekechea na shule za msingi hadi sekondari. Ni vyema ujuzi kuhusu taaluma ya ushairi uanzie viwango vya chini kwenda juu kwani; samaki mkunje angali mbichi.

## Hitimisho

Makala haya yameshughulikia changamoto za ufasiri wa ushairi na uelewekaji wa ushairi miongoni mwa wasomi katika kiwango cha sekondari kwa kuangazia suala la athari za umilisi kimsingi wa ushairi. Kila msomi anatarajiwa kuwa na umilisi kimsingi katika taaluma anayoishughulikia. Wasomi wa ushairi huchukuliwa kwamba wana umilisi kimsingi kuhusu ushairi kwa kila kiwango cha usomi. Fikra na dhana hii kama tulivyokwisha kuona, yaweza au isiweze kuwa na ukweli. Kwa wasomi wenye mapungufu ya umilisi kimsingi wa ushairi, mambo huenda kinyume na matarajio. Wao hukosa kumakinika na hili huibua mielekeo hasi kuhusu ushairi na matokeo ya mitihani yasiyo ya kurithisha. Hili hutamausha na kupunguza adhama ya ushairi kama utanzu wa fasihi ya Kiswahili. Tumeeleza umilisi huo kwa njia mbili. Ya kwanza ni upungufu katika kiwango cha awamu ya usomi na ya pili ni upungufu unaoweza kuhusishwa na hatua za usomaji na ujifundishaji. Upugufu unaohusishwa na hatua za usomaji na usomi wa taaluma ya ushairi huweza kutokea katika viwango vyovyote vile vya usomi wa taaluma ya ushairi. Mapungufu haya mawili yapaswa kukabiliwa ili kuboresha ufasiri na uelewekaji wa ushairi miongoni mwa wasomi hao. Upungufu huu huathiri mstakabali wa ufasiri wa ushairi kwa vizazi vinavyofuatia. Njia mojawapo ya kukabiliana nayo ni kutanguliza masomo ya ushairi katika viwango vya kimsingi vya elimu kama vile chekechea, shule ya msingi na kidato cha kwanza na cha pili. Hii itakuwa njia bora ya kuwafaa wanafunzi wa sekondari ambao ndio nguzo ya ufunzaji ushairi wa Kiswahili kesho.

**Marejeleo**

Chacha, N. (1987). 'The Meaning and Interpretation of Swahili Poetry'. Ph.D Thesis.Yale University.

Daiches, D. (1956). *Critical Approaches to Literature*. London: Longman.

Davis, R. na R. Schleifer (1986) *Contemporary Criticism: Literary & Cultural Studies*. Longman: London.

Derida, J. (1976). *Of Grammatology*. Baltimore, M.D. (Tafsiri kutoka De la grammatologie, Paris: 1967).

Foucalt, M. (1972). The Archeology of Knowledge and the Discourse of Language. New York: Routledge Publishers

Gakuo, J. (2014). "Changamoto za uchanganuzi na ufasiri wa ushairi katika shule za upili nchini Kenya". Tasnifu ya PhD, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Gibbe, A. (1978). 'Fasihi na Jamii, Baadhi ya Washairi wa Kiswahili – 1960 – 1977' katika Jarida la TUKI – KISWAHILI.

Gibbe, A. (1980). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Dar es Salaam, Tanzania Publishing House.

Gibbe, A. (1990). 'Ufumbaji na Ufumbuaji wa Mashairi' Jarida la Kiswahili. Dar es Salaam: Education Service Centre Ltd.

Hirsch, E. (1987). *Contexts for Criticism*. Mayfield Publishing Company Mountain View, California London. Toronto.

Kezilahabi, E. (1982). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kimaru, H. (2010). *Taifa Leo*, Jumanne Agosti 2010, Nation Media Grup, Nation Centre, Nairobi.

King'ei, K. (2000). *Miale ya Uzalendo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Masinde, E. (2007). *Ufundishaji wa Ushairi katika Shule za Upili na Vyuo*. Taaluma: Nairobi.

Massamba, D. (2003). "Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili". Makala ya Semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kiswahili.

Ministry of Education, Science and Technology (2002), 2003, 2004 KCSE: Fasihi ya Kiswahili 102/3 Report.

Mulokozi, M. (1975). '*Revolution and Reaction in Swahili Poetry*' katika KISWAHILI Juzuu 45/2.Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TUKI.

Murfin, R. (1991). *Case Studies in Contemporary Criticism*. New York: St. Martins Press.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Rice, P et al. (1983). *Case Studies in contemporary Criticism*. New York: St. Martins Press.

Ricoeur, P. (1976). *Interpretation Theory: Discourse and the Surplus of Meaning*. Texas Christian University Press.

Robert, S. (1972). *Sanaa ya Ushairi*. Nairobi: Thomas, Nelson and Sons.

Senkoro F. (1988). *Shairi Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: University Press.

Syambo, B. na Mazrui A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Publishers.

Waititu, F. na wenzake (2003). Kiswahili Fasaha, kidato cha Kwanza: kitabu cha wanafunzi. Nairobi: Oxford University press.

Waititu, F. na wenzake (2003). Kiswahili Fasaha, kidato cha pili: kitabu cha wanafunzi. Nairobi: Oxford University press.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*, *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.

Wellek, R. na Warren, A. (1949). *Theory of Literature*. Harmondsworth: Penguin Books Limited.